# SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA WAKALA


3. Kuanzishwa kwa Wakala.

4. Uwezo na malengo ya Wakala.

5. Muhuri wa Wakala.

6. Kazi za Wakala.


### SEHEMU YA TATU
### UONGOZI WA WAKALA


7. Bodi ya Wakurugenzi.

8. Sifa za Mwenyekiti.

9. Kazi za Bodi.

10. Kamati za Bodi.

11. Kukasimu kazi za Bodi.

12. Vikao vya Bodi.

13. Akidi ya Kikao cha Bodi.

14. Maamuzi ya Bodi.

15. Kumbukumbu za vikao vya Bodi.

16. Taratibu za vikao.

17. Kujiuzulu kwa mjumbe.

18. Kuondoshwa au kusitishwa kwa mjumbe.

19. Posho za wajumbe.

20. Mjumbe mualikwa.

**SEHEMU YA NNE**
**MKURUGENZI MTENDAJI NA WAFANYAKAZI WENGINE WA WAKALA**

21. Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

22. Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

23. Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.

24. Wafanyakazi wa Wakala.

25. Kurugenzi za Wakala.

26. Uwezo wa Waziri na uhusiano wake na Wakala.

27. Uhusiano baina ya Wakala na Wizara.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI YA FEDHA**

28. Fedha za Wakala.

29. Makadirio ya mapato na matumizi.

30. Hesabu na ukaguzi.

31. Ripoti ya mwaka ya utekelezaji.

32. Ufunguaji wa Hesabu ya Benki.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU


33. Makosa yanayohusiana na Wakala.


## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA JUMLA


34. Kinga.

35. Kuhaulisha mali.

36. Wajibu wa Taasisi za Serikali.

37. Kanuni.

38. Kufuta na kubakiza.

**SHERIA NAM 2 YA 2019**

**NIMESAINI**

Ashein

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

7 Mei ..........................................., **2019**

# SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo, 2019 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ulioanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Kilimo" maana yake ni mazao yanayolimwa ardhini, misitu na rasilimali zinazotokana na mazingira yoyote ya uoteshaji;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 7(1) cha Sheria hii;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 21(1) cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya huduma za matrekta na zana za kilimo;

"Wizara" maana yake ni Wizara inayohusika na masuala ya huduma za matrekta na zana za kilimo;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Kitengo" maana yake ni kitengo cha Karakana ya matengenezo ya matrekta.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA WAKALA

Kuanzishwa kwa Wakala.

**3.** Kunaanzishwa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo.

Uwezo na malengo ya Wakala.

**4.**-(1) Wakala utakuwa ni mamlaka isiyojitegemea, kwa muundo na hadhi yake utakuwa na uwezo ufuatao:

(a) kupata, kumiliki, kununua au kuhamisha mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika;

(b) kuingia kwenye mkataba wowote, ubia au muamala kwa mujibu wa Sheria;

(c) kukopa fedha kutoka katika taasisi yoyote ya kifedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(d) kutekeleza au kufanya jambo lolote au kitu chochote ambacho Wakala wa aina yake unaweza kutekeleza kwa mujibu wa Sheria.

(2) Wakala utakuwa na malengo ya:

(a) kuwa na Karakana za matengenezo ya matrekta zilizosheheni vifaa vyenye uwezo wa kutosha katika kukabiliana na soko la zana za kilimo;

(b) kuongeza uzalishaji wa kilimo chenye tija, faida na kipato kinachotokana na ongezeko la uwekezaji katika utumiaji wa zana za kilimo kupitia ushirikishwaji mkubwa wa sekta binafsi na kuimarisha utoaji wa huduma bora za matrekta na zana za kilimo kwa jamii;

(c) kuongeza ufanisi katika kutoa huduma bora za matrekta na zana za kilimo kwa wakulima, kupunguza ugumu katika kazi za kilimo na kufanya kazi za kilimo mashambani kuwa zenye kuvutia; na

(d) kuendeleza programu zenye ufanisi katika uongozi na utawala.

Muhuri wa Wakala.

**5.**-(1) Kutakuwa na muhuri wa Wakala katika muundo na aina kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Nyaraka yoyote itakayotolewa na Wakala itawekwa muhuri wa Wakala na itathibitishwa kwa sahihi ya Mkurugenzi Mtendaji au Ofisa mwengine wa Wakala aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji.

(3) Kutakuwa na kifupisho cha Wakala kama itakavyoamuliwa na Bodi.

Kazi za Wakala.

**6.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Wakala utakuwa na kazi za:

(a) kuendeleza na kukuza huduma za ukodishaji wa matrekta kwa wakulima, sekta binafsi na taasisi mbali mbali katika matumizi bora ya matrekta pamoja na zana nyengine katika kilimo;

(b) kuendesha biashara ya ununuzi wa matrekta, kuunganisha matrekta na zana zake husika, kusafirisha na kuingiza matrekta na zana za kilimo zilizokwishaunganishwa na kuwa kama wazalishaji, wakala wa mauzo wa zana za kilimo na vifaa vyenginevyo kama vinavyohitajika na wateja;

(c) kuendeleza utoaji wa huduma za matengenezo makubwa na ya kawaida ya matrekta, zana zake pamoja na zana nyengine za kilimo;

(d) kuendeleza utafiti unaohusiana na matumizi ya zana za kilimo kwa lengo la kuongeza ufahamu kwa wakulima na uelewa wa kujua aina na uwezo wa matrekta na zana za kilimo zitakazohitajika kulingana na aina mbali mbali za udongo;

(e) kutoa mafunzo ya kiufundi kwa wafanyakazi wa Wakala kuhusu matrekta, zana za matrekta na zana za kilimo kwa ajili ya kupata taaluma na ujuzi kuwezesha usimamizi bora;

(f) kutoa mafunzo kwa wahandisi, mafundi na watumiaji wa matrekta, wasimamizi wa zana za kilimo, madereva wa matrekta, waendeshaji wa zana nyengine za kilimo katika kuwawezesha kujifunza na kupata uzoefu utakaowafaa katika kuhudumia matrekta na zana za kilimo; na

(g) kufanya kazi nyengine yoyote chini ya Sheria hii au itakayokuwa na umuhimu katika kufikia malengo ya Wakala.

## SEHEMU YA TATU
## UONGOZI WA WAKALA

Bodi ya Wakurugenzi.

**7.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mtendaji;

(c) Mkurugenzi anayehusika na Kilimo;

(d) Mkurugenzi wa Karakana Kuu ya Serikali; na

(e) Wajumbe watatu watakaoteuliwa na Waziri mmoja kati yao kutoka katika Jumuiya za Wakulima.

(2) Ukitoa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia jinsia na taaluma.

(3) Bodi itamteua mmoja miongoni mwa wajumbe kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

(4) Mwenyekiti wa Bodi atatumikia nafasi kwa kipindi cha miaka minne kutoka tarehe ya uteuzi wake na anaweza kuwa na sifa ya kuteuliwa tena.

(5) Ukitoa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine wa Bodi watatumikia nafasi kwa miaka mitatu na wanaweza kuwa na sifa ya kuteuliwa tena.

(6) Bodi itamteua mwanasheria mwenye sifa ndani ya Wizara au Wakala kuwa Katibu wa Bodi.

(7) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki, Katibu atawajibika kwa Bodi, na atawajibika kuhakikisha kuwa:

(a) kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi zinachukuliwa kwa umakini;

(b) kumbukumbu sahihi na zinazojitosheleza za Bodi zinahifadhiwa kwa umakini;

(c) taarifa sahihi za vikao vya Bodi zinatolewa kwa wajumbe; na

(d) anatoa ushauri sahihi kwa Bodi wakati inapohitajika, na mambo mengine kama Bodi itakavyoagiza.

Sifa za Mwenyekiti.

**8.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti iwapo mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya uhandisi wa kilimo, uhandisi wa zana za kilimo au fani nyengine zinazohusiana na fani hizo kutoka chuo kikuu kinachotambulika;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka kumi katika fani ya uhandisi wa kilimo au fani zinazohusiana na hizo;

(d) ana heshima ya kiwango cha juu katika utumishi wa umma; na

(e) ana uwezo wa kiwango cha juu wa kusimamia kwa ufanisi na ubora masuala ya Wakala.

Kazi za Bodi.

**9.** Bodi itakuwa na kazi za:

(a) kusimamia na kuendesha uongozi wa Wakala katika kutekeleza majukumu yake ya utoaji wa huduma za matrekta na zana za kilimo;

(b) kupitia na kuridhia sera, mipango ya kibiashara na uendeshaji, ukaguzi na ripoti za kifedha, na taarifa za Wakala kulingana na malengo ya Wakala yaliyomo chini ya Sheria hii;

(c) kuweka miongozo juu ya utekelezaji wa mpango mkakati wa Wakala na kuidhinisha bajeti ya kila mwaka;

(d) kupendekeza muundo wa kuanzishwa kwa Idara au Vitengo au divisheni za Wakala pale itakapohitajika kulingana na taratibu za Kamisheni ya Utumishi wa Umma;

(e) kumshauri Waziri njia bora ya kuendeleza Wakala;

(f) kuweka miongozo sahihi ya kisera, mipango ya kibiashara na kiuendeshaji pamoja na utekelezaji wa bajeti;

(g) kusaidia utayarishaji wa malengo yaliyopendekezwa, viashiria vya utekelezaji wa majukumu ya Wakala kama ilivyokubaliwa kulingana na:

(i) mpango mkakati wa Wakala; na

(ii) mpango kazi wa mwaka wa Wakala.

(h) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo imeainishwa katika Sheria hii ambayo inaweza kuwa ni muhimu katika kufikia malengo ya kuanzishwa kwa Wakala.

Kamati za Bodi.

**10.** Bodi inaweza, kwa makubaliano na masharti kama itakavyoamua, kuanzisha Kamati, kama itakavyoona kuna umuhimu wa kufanya kazi.

Kukasimu kazi za Bodi.

**11.** Bodi inaweza, ikiona inafaa kwa utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati au Katibu wa Bodi.

Vikao vya Bodi.

**12.**-(1) Bodi itafanya vikao vyake vya kawaida angalau mara moja katika kila kipindi cha miezi mitatu na inaweza kukutana ikiwa ipo haja ya kufanya hivyo kwa kutekeleza kazi zake katika maeneo kama Bodi itakavyoamua kila baada ya muda.

(2) Kikao cha Bodi kitaitishwa na kuendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa Mwenyekiti hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao na ikiwa wote wawili Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliopo katika kikao watamteua mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi ya Kikao cha Bodi.

**13.** Akidi ya kikao cha Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya Wajumbe wa Bodi kwa kila kikao.

Maamuzi ya Bodi.

**14.**-(1) Maamuzi ya Bodi yatafanywa kwa makubaliano na ikiwa makubaliano hayatofikiwa, maamuzi yatafanyika kwa kupiga kura na endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti au mjumbe anayeendesha kikao atakuwa na kura ya maamuzi.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, maamuzi yanaweza kufanywa na Bodi kwa kupitisha karatasi kwa wajumbe ambapo kila mjumbe ataelezea maoni yake kwa maandishi isipokuwa kwamba mjumbe yeyote anaweza kuhitaji kuwa uamuzi wowote ubatilishwe kwa kujadiliwa katika kikao kamili cha Bodi.

(3) Maazimio ya maandishi yanayotokana kwa kupitisha karatasi kwa wajumbe na kusainiwa na wajumbe wote waliopo Zanzibar lakini wajumbe hao hawatapungua watano, yatachukuliwa kama ni maamuzi yaliyofanywa katika kikao isipokuwa kwamba mjumbe anaweza kuhitaji, bila ya kujali saini za wajumbe, jambo hilo lipelekwe katika kikao cha Bodi kinachofuata.

Kumbukumbu za vikao vya Bodi.

**15.** Kumbukumbu za uendeshaji wa vikao vyote vya Bodi zitathibitishwa katika kikao kinachofuata cha Bodi na kuwekwa saini na Mwenyekiti wa kikao na Katibu wa Bodi.

Taratibu za vikao.

**16.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuweka taratibu zake zinazohusiana na vikao na uendeshaji bora wa kazi zake ikijumuisha Kamati za Bodi.

Kujiuzulu kwa mjumbe.

**17.** Mwenyekiti au mjumbe yeyote wa Bodi anaweza, wakati wowote kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi ya mwezi mmoja kwa mamlaka ya uteuzi na kutoka tarehe iliyoainishwa katika taarifa au, ikiwa tarehe haijaainishwa kutoka tarehe iliyopokelewa taarifa hiyo na mamlaka ya uteuzi, atasita kuwa mjumbe.

Kuondoshwa au kusitishwa kwa mjumbe.

**18.** Waziri anaweza kumuondosha au kumsitisha mjumbe yeyote wa Bodi asiyekuwa Mwenyekiti na Mjumbe anayeingia kwa nafasi yake ikiwa mjumbe huyo:

(a) hana uwezo wa kutekeleza kazi katika nafasi yake kwa sababu za kiafya za kimwili au kiakili;

(b) ametiwa hatiani kwa kosa la jinai linalohusiana na udanganyifu, kutokuwa mwadilifu au kinyume na maadili;

(c) amejiuzulu;

(d) amefariki;

(e) ameshindwa kuhudhuria katika vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya kuwa na ruhusa ya Mwenyekiti; au

(f) kwa sababu nyengine yoyote ya msingi itakayotolewa kwa maandishi.

Posho za wajumbe.

**19.** Wajumbe wa Bodi watalipwa posho kama Waziri atakavyoamua kila baada ya muda kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Kanuni na Miongozo.

Mjumbe mualikwa.

**20.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote asiyekuwa mjumbe kuhudhuria katika kikao chochote cha Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa, hatokuwa na haki ya kupiga kura.

## SEHEMU YA NNE
## MKURUGENZI MTENDAJI NA WAFANYAKAZI WENGINE WA WAKALA

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

**21.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji atakayeteuliwa na Rais.

(2) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala na atawajibika kwa kazi za kila siku za Wakala.

Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

**22.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji iwapo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza kutoka katika chuo kikuu kinachotambulika katika fani ya uhandisi wa kilimo, uhandisi wa zana za kilimo au fani nyengine zinazohusiana na fani hizo;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka saba katika fani ya Uhandisi wa Kilimo au fani zinazohusiana na hizo; na

(d) ana heshima ya kiwango cha juu katika utumishi wa umma.

Majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji.

**23.** Mkurugenzi Mtendaji atakuwa na majukumu ya:

(a) kuwajibika kwa shughuli za kila siku;

(b) kuwajibika kwa mapato yote na matumizi ya Wakala;

(c) kusimamia mambo ya Wakala kwa ufanisi na gharama stahiki;

(d) kusimamia huduma za matrekta na zana nyengine za kilimo na makubaliano mengine ya kimataifa yanayohusiana na masuala ya zana za kilimo;

(e) kusimamia mapato yote, matumizi na makusanyo ya Wakala kwa mujibu wa sheria husika;

(f) kuangalia na kuimarisha ufanisi wa kazi zote za Wakala za:

(i) usimamizi wa kazi za kila siku za Wakala; na

(ii) usimamizi wa fedha, mali na kazi za Wakala.

(g) kuwasilisha taarifa za kazi za Wakala kwa Bodi; na

(h) kutekeleza majukumu mengine yoyote kama itakavyolazimika au kuhitajika kwa utekelezaji mzuri wa kazi chini ya Sheria hii.

Wafanyakazi wa Wakala.

**24.**-(1) Bodi inaweza, kwa makubaliano na masharti, kuajiri wafanyakazi wengine, au kuajiri huduma za ushauri elekezi au utaalamu, kama itakavyohitajika kwa utekelezaji mzuri wa kazi za Wakala.

(2) Uajiri wa wafanyakazi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utafanywa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

(3) Wafanyakazi waliopo katika kitengo wataendelea kufanya kazi na watachukuliwa ni wafanyakazi wa Wakala walioajiriwa chini ya masharti ya Sheria hii.

Kurugenzi za Wakala.

**25.**-(1) Ndani ya Wakala kutakuwa na Idara, Kitengo na Divisheni kama itakavyohitajika kwa utekelezaji mzuri wa kazi zake kama itakavyoamuliwa na Bodi na kuidhinishwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

(2) Mkuu wa Idara atateuliwa na Bodi, na atakuwa mtu mwenye elimu na uzoefu wa kutosha kutekeleza kazi za Idara husika.

(3) Mkuu wa Idara, Kitengo na Divisheni atatekeleza kazi zake chini ya usimamizi wa Mkurugenzi Mtendaji.

Uwezo wa Waziri na uhusiano wake na Wakala.

**26.** Katika kutekeleza kazi zake, Waziri atakuwa na uwezo wa kusimamia utekelezaji wa Sera zinazohusiana na Wakala na kutoa maelekezo ya jumla na amri kwa Wakala na Bodi kama atakavyoona inafaa.

Uhusiano baina ya Wakala na Wizara.

**27.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Wakala utakuwa na wajibu wa kuwasilisha taarifa yoyote ya utawala na utendaji kwa Wizara kama itakavyohitajika.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Wakala.

**28.**-(1) Fedha na rasilimali za Wakala zitajumuisha:

(a) fedha zilizotengwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya matumizi ya Wakala;

(b) fedha zilizopokelewa na Wakala kutokana na bidhaa au huduma zilizotolewa na Wakala;

(c) misaada halali, zawadi, michango, mikopo, urithi, au uwekezaji ambao unaweza kupokelewa kutoka kwa mtu yeyote au jumuiya; na

(d) fedha nyengine zozote itakazopewa au kupatikana kihalali na Wakala.

(2) Wakala utatekeleza kazi zake kwa mujibu wa misingi ya kifedha inayotambulika na utahakikisha kwamba, kadri iwezekanavyo, makusanyo yake yanatosheleza kukidhi matumizi sahihi kwa mujibu wa mpango mkakati.

(3) Stakabadhi zote na mapato yatakuwa ni mali ya Wakala na kwa kuzingatia uwezo wa Wakala wa kuongeza mapato kutoka katika utendaji kazi wake na uwezo wake wa kujitegemea kifedha, athari ya kifedha ya mpango wake mkakati na mpango wa mwaka wa kazi na bajeti.

(4) Waziri anaweza baada ya kushauriana na Waziri wa Fedha, kuamua kiwango cha makusanyo ambacho kitabakia kuwa mali ya Wakala na kiwango cha makusanyo ambacho kitachukuliwa kuwa ni fedha za umma na kuwekwa katika hesabu ya Serikali.

(5) Miamala yote ya fedha ya Wakala itafanywa na kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine za fedha.

Makadirio ya mapato na matumizi.

**29.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala atatayarisha au kusababisha kutayarishwa, si chini ya miezi mitatu kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka unaofuata na anaweza, wakati wowote kabla ya mwisho wa mwaka.

(2) Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa Wakala yatawasilishwa kwa Bodi kwa mazingatio na baada ya hapo, yatawasilishwa kwa Waziri anayehusika kwa ajili ya kuidhinishwa.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, makadirio ya mapato na matumizi yatajumuisha makadirio ya ziada.

(4) Makadirio ya mapato na matumizi ya Wakala yatatayarishwa kwa mujibu wa matakwa na masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na maagizo mengine kama yatakavyoweza kutolewa na Serikali kila baada ya muda.

(5) Mkurugenzi Mtendaji atahakikisha kwamba malipo yote ya fedha za Wakala yanalipwa kwa usahihi na yanaidhinishwa ipasavyo na udhibiti unaopaswa unazingatiwa kwa mali zake na madeni ya Wakala

Hesabu na ukaguzi.

**30.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala atahakikisha kwamba vitabu vya hesabu na kumbukumbu nyengine za fedha katika utekelezaji wa kazi za Wakala zinahifadhiwa ipasavyo kwa mujibu wa utaratibu wa fedha za umma na uhasibu.

(2) Hesabu za Wakala zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mkaguzi mwengine aliyesajiliwa na kuidhinishwa kwa madhumuni hayo na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama atakavyoamua.

Ripoti ya mwaka ya utekelezaji.

**31.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala, ndani ya kipindi cha miezi miwili baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, atatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka kuhusiana na mwaka huo wa fedha ikijumuisha:

(a) nakala ya hesabu zilizokaguliwa za Wakala, pamoja na ripoti ya mkaguzi kuhusiana na hesabu hizo;

(b) ripoti ya utekelezaji wa kazi na taarifa nyengine zinazohusiana;

(c) ripoti ya Wakala ya mwaka wa fedha uliokamilika; na

(d) taarifa nyengine kama Waziri atakavyohitajia.

(2) Waziri atahakikisha kwamba nakala ya ripoti ya mwaka ya Wakala inawasilishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi, ndani ya miezi miwili au katika kikao kinachofuata cha Baraza la Wawakilishi baada ya kupokea ripoti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Ufunguaji wa Hesabu ya Benki.

**32.** Wakala unaweza, baada ya kupata ruhusa ya Waziri mwenye dhamana ya fedha na kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, kufungua hesabu katika Benki yoyote kwa ajili ya kuweka fedha zake na kuendesha hesabu hiyo kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mujibu wa Sheria.

## SEHEMU YA SITA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa yanayohusiana na Wakala.

**33.** Mtu ambaye:

(a) bila ya ruhusa ya kisheria, anafanya shughuli yoyote ya kiufundi, anazuia zana, anawasiliana na mtu yeyote asiyekuwa katika utekelezaji

wa majukumu yake ya kikazi au anatoa taarifa alizozipata kutokana na ajira yake;

(b) kutokana na nafasi yake ya ajira, anamiliki na kutumia taarifa yoyote inayohusiana na kazi za Wakala, zana au malighafi kwa maslahi yake binafsi;

(c) anatoa siri, taarifa za uongo au za kupotosha kuhusiana na kazi za Wakala;

(d) anauza, anatumia, anaiba au anaruhusu mashine za Wakala kutumika bila ya ruhusa ya Wakala;

(e) anamruhusu mtu yeyote kutoka nje ya kiwanda kutumia muhuri, nembo, mashine na zana nyenginezo bila ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji;

(f) anatumia, anasaidia au anaruhusu muhuri, nembo, mashine na zana nyengine za Wakala kutumika bila ya ridhaa ya Mkurugenzi Mtendaji; au

(g) anakwenda kinyume au anashindwa kufuata sharti lolote la Sheria hii,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tatu au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja au vyote viwili faini na kifungo.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI MENGINEYO

Kinga.

**34.** Mjumbe wa Bodi, mfanyakazi au mtu yeyote aliyeajiriwa na Wakala hatowajibika yeye binafsi kwa jambo lolote au kitu alichokifanya au ameacha kukifanya kwa nia njema wakati wa utekelezaji wa kazi zake ndani ya mazingira ya kazi au utekelezaji wa jukumu lake chini ya Sheria hii.

Kuhaulisha mali.

**35.** Mali na madeni ambayo yapo kwa Wakala kabla ya Sheria hii, baada ya kuanza kutumika Sheria hii yatakuwa ya Wakala pamoja na riba, madeni, tozo, majukumu na dhamana zake zinazoathiri mali hizo.

Wajibu wa Taasisi za Serikali.

**36.**-(1) Wakala unaweza, baada ya kuombwa, kuwa na wajibu wa kutoa huduma zake kwa Wizara, Idara, Mamlaka, Mashirika na Taasisi nyengine za Serikali na Wizara, Idara, Mamlaka, Mashirika na Taasisi hizo nyengine za Serikali zitawajibika kuomba ushauri wa kiufundi kwa Wakala.

(2) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na bila ya kujali masharti ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Taasisi za Serikali zitawajibika kufuata taratibu za manunuzi zinazoelekezwa.

Kanuni.

**37.**-(1) Waziri anaweza, kwa kushauriana na Bodi, kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza, kwa madhumuni maalum, kutunga Kanuni juu ya mambo yafuatayo:

(a) kupata nyaraka na taarifa zilizowekwa na Wakala; na

(b) uvunjwaji wa masharti yaliyowekwa chini ya kifungu cha 36 cha Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**38.**-(1) Tangazo la Kisheria Nam. 55 la 2017 linafutwa.

(2) Bila ya kujali ufutwaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa au lililotarajiwa kufanywa chini ya Tangazo la Kisheria lililofutwa, litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 7 Februari, 2019.

..............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.***